




Hashim anapenda maembe.
Huu msimu wa joto, maembe yako karibu kuharibika.
Hashim anataka kuyaokoa.



Baba akamwambia Hashim yakwamba akitoa maji kutoka kwa maembe, hayata haribika.
Chembi chembi za uchafu zinazo sababisha maradhi haziwezi kuishi bila maji," akasema.





"Tutawezaje kutoa maji kwa maembe?".
akauliza Hashim.
"Ongeza chumvi ndani!" akasema Baba.

Basi Baba na Hashim wakaweka maembe nje kwa jua yakauke.



Waka weka maembe ndani ya chupa pamoja na mafuta.
Mafuta hayawezi kuruhusu uchafu kutoka kwa hewa kufikia
maembe.



"Baba, tume tengeneza kachumbari!". akasema Hashim.




Tutawezaje kuhifadhi matunda na mboga tunazo zipenda?





Kipande cha viazi + Chemsha + kausha = vipanzi vya viazi
(kukaangwa na kuliwa)





Nyanya + chumvi + jua + mafuta = nyanya kavu

